**MAELEZO MAFUPI YA BALOZI MHANDISI JOHN W.H. KIJAZI, MWENYEKITI WA BODI YA USHAURI YA WAKALA WA NDEGE ZA SERIKALI (TGFA) WAKATI WA UZINDUZI WA BODI YA USHAURI ULIOFANYIKA TAREHE 19 MEI, 2020, IKULU, CHAMWINO DODOMA**

---

**Mheshimiwa Kapteni Mstaafu George Huruma Mkuchika (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora;**
**Katibu Mkuu Ikulu;**
**Wajumbe wa Bodi ya Ushauri ya Wakala wa Ndege za Serikali;**
**Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Ndege za Serikali;**
**Watumishi wa Wakala wa Ndege za Serikali mliopo;**
**Mabibi na Mabwana.**

Habari za asubuhi.

Napenda nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kukutana leo kwa mara ya kwanza kwa ajili ya uzinduzi rasmi wa Bodi hii ya Wakala wa Ndege za Serikali (TGFA) na baadae kufanya kikao cha kwanza cha Bodi.

Aidha, napenda kukushukuru sana wewe Mheshimiwa Waziri, kwa kutenga muda wako kwa ajili ya shughuli hii. Sote tunafahamu kwamba

kikao cha Bunge bado kinaendelea, hivyo unayo majukumu mengi katika kipindi hiki.

Nachukua nafasi hii pia kuwapongeza Wajumbe wa Bodi hii kwa kuteuliwa kwenu kuhudumu katika Bodi ya Ushauri ya Wakala wa Ndege za Serikali kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia tarehe 26 Februari, 2020. Hongereni na karibuni tusaidiane kwa pamoja katika kutekeleza jukumu tulilopewa.

**Mheshimiwa Waziri,** kwa niaba ya Wajumbe wa Bodi hii, na kwa niaba yangu binafsi, napenda pia kuchukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa **Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,** pamoja na wewe mwenyewe, kwa kutuamini na kutukabidhi jukumu hili la kuisimamia taasisi hii ambayo uzito wa majukumu yake umeongezeka sana kufuatia hatua zinazochukuliwa na Serikali ya Awamu ya Tano za kuimarisha usafiri wa anga, hususan kuimarisha Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) kwa kununua ndege mpya na kuzikodisha kwa Kampuni hiyo.

**Mheshimiwa Waziri,** Wajumbe wa Bodi hii tunatambua **unyeti na umuhimu wa majukumu ya TGFA**. Kwa hiyo tunatambua uzito wa jukumu tulilopatiwa kama Bodi. Kwa niaba ya Wajumbe wa Bodi hii, naomba nikuhakikishie kwamba tutaisimamia TGFA kikamilifu ili kuhakikisha kwamba inatekeleza wajibu wake wa kufanikisha mipango ya Serikali katika kuimarisha sekta ya usafiri wa anga, ikiwa ni pamoja na

kuhakikisha kwamba Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na Viongozi Wakuu wa Kitaifa wanapatiwa huduma bora na salama ya usafiri wa anga, ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao ya kitaifa na kimataifa kwa ufanisi mkubwa. Katika kufanya kazi yake, Bodi itazingatia **weledi, sheria**, **kanuni** na **miongozo ya Serikali**.

**Mheshimiwa Waziri,** kama unavyofahamu, tangu mwezi Septemba, 2016 hadi sasa Serikali imenunua ndege mpya nane (8) na kuzikodisha kwa ATCL kwa makubaliano ya malipo ya kila mwezi kwa kila ndege kutegemea aina na uwezo wa ndege husika. Kwa sasa Serikali imeagiza ndege nyingine mpya tatu (3) ambazo awali zilitarajiwa kuwasili nchini kati ya Juni, 2020 na Juni, 2021, lakini kutokana na athari za Covid – 19, ufuatiliaji unaendelea kufanyika ili kupata ratiba mpya ya kuwasili ndege hizo. Taarifa za awali ni kuwa sasa itawasili mnamo Desemba, 2020.

Hata hivyo, kumekuwa na changamoto kwa ATCL kushindwa kutekeleza majukumu yake ya kuwasilisha malipo yote ya fedha kwa TGFA kwa mujibu wa mikataba iliyosainiwa. Ili kushughulikia suala hili, niliwaagiza Katibu Mkuu, Ikulu na Katibu Mkuu (Uchukuzi) waandae kikao cha Mawaziri wao ili changamoto hii iweze kupatiwa ufumbuzi. Bodi itafuatilia kwa karibu suala hili na kuhakikisha kuwa linapatiwa ufumbuzi haraka.

**Mheshimiwa Waziri,** pamoja na **changamoto ya malipo ya ukodishaji wa ndege**, changamoto nyingine inayoikabili TGFA ni pamoja na

**uchakavu wa hanga la ndege; na ugumu wa kufanya matengenezo ya ndege za zamani** (ambazo ni aina ya Fokker 28 na PIPER NAVAJO). Ugumu huo unatokana na watengenezaji wa ndege kusitisha uzalishaji wa aina hizo za ndege, na hivyo kusababisha upatikanaji wa vipuri vya ndege hizo kuwa mgumu. Changamoto nyingine ni **uchache wa watalaam hususan wahandisi wa ndege** (*certified aircraft maintenance engineers)* wanaotambulika kimataifa. Pamoja na shughuli nyingine, Bodi itajielekeza katika kuhakikisha kuwa changamoto nilizozitaja zinatafutiwa ufumbuzi.

**Mheshimiwa Waziri**, vilevile katika miezi ya hivi karibuni, imejitokeza **changamoto ya janga la ugonjwa wa Covid-19**. Sekta ya usafiri wa anga ni moja ya sekta zilizoathirika sana na janga hili. **Mapato ya TGFA yanayotokana na ukodishaji wa ndege yanatarajiwa kushuka sana kutokana na athari ambazo ATCL wamepata**. Ni matumaini yetu kwamba janga hili halitadumu kwa muda mrefu zaidi ili ATCL irejee katika kutekeleza mipango yake ya kibiashara kama ilivyopangwa awali.

**Mheshimiwa Waziri**, baada ya kusema haya, naomba sasa nikukaribishe ili uweze kuzungumza na Bodi hii ya Ushauri ya Wakala wa Ndege za Serikali, na kisha kuizindua rasmi. Aidha, Bodi ipo tayari kupokea maelekezo ya Serikali yatakayokuwa dira katika utekelezaji wa majukumu yake.

Kabla sijakukaribisha ili utoe nasaha zako kwa Bodi naomba kwanza nichukue nafasi hii kuwakaribisha Wajumbe wa Bodi pamoja na Mtendaji Mkuu wa TGFA (ambae pia ni Katibu wa Bodi hii) wajitambulishe kwako.

**Karibu sana Mheshimiwa Waziri.**